**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA KUMI NA TANO

**09 MEI, 2016**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA KUMI NA TANO – TAREHE 09 MEI, 2016

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

## II. MASWALI:

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**120. MHESHIMIWA CECIL DAVID MWAMBE (NDANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga wodi ya wazazi (*Maternity ward*) kwenye kituo cha Afya Chiwale kwa kuwa wazazi hujifungulia kwenye chumba kilichomo ndani ya jengo ambalo pia hutumika kulaza wagonjwa wa kiume na kike.

**121. MHESHIMIWA RIZIKI SHAHARI MNGWALI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kwa mila zetu za kiafrika, imezoeleka kuwa huduma ya ukunga kwa kina mama wajawazito wakati wa kujifungua hutolewa na wataalamu wanawake:-

Je, Serikali haioni kuwa kwa kuweka wakunga wanaume katika baadhi ya Zahanati za Serikali nchini ni kuwadhalilisha akina mama wajawazito wanaojifungua katika zahanati hizo.

**WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

**122. MHESHIMIWA BALOZI ADADI MOHAMED RAJAB (MUHEZA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Wilaya ya Muheza ina utajiri wa uzalishaji wa Matunda kama Machungwa, Maembe, Machenza, Mafenesi n.k.:-

Je; ni lini Serikali itajenga kiwanda Wilayani hapo cha kutengeneza juisi na kuwaondolea usumbufu Wakulima hao wa kutafuta soko.

## WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, WASANII NA MICHEZO:

### 123. MHESHIMIWA MARTHA JACHI UMBULLA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Wasanii na Michezo:- Ujenzi wa Senta ya michezo ya riadha katika Mkoa wa Manyara hususan Wilaya ya Mbulu imekuwa ni kilio cha muda mrefu kwa viongozi na Wananchi wa eneo husika kutokana na vijana wengi kuwa na vipaji katika mchezo wa riadha na michezo mingine:-

(a) Je, ni lini Serikali itasikiliza kilio hicho cha muda mrefu na kujenga senta ya michezo ya riadha mkoani Manyara ili vijana wengi wenye vipaji waweze kunufaika;

(b) Je, Serikali haioni kuwa kwa kujenga senta ya michezo Manyara itaweza kupunguza changamoto ya ukosefu wa ajira kwa vijana wa mkoa huo na maeneo jirani kama Singida, Arusha na Dodoma ambako kuna vipaji hivyo.

## WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

### 124. MHESHIMIWA INNOCENT LUGHA BASHUNGWA (KARAGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Kwa miaka mingi sasa Tanzania Investment Bank na TADB imekuwepo ila mchango wake katika kupunguza umasikini haufahamiki zaidi hata kwa waheshimiwa wabunge:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa bank za TIB na TADB zinajielekeza kwenye utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa sababu ndiyo mkataba wa mpango kazi wa maendeleo ya nchi yetu.

### 125. MHESHIMIWA OMARI MOHAMED KIGUA (KILINDI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Ulipaji kodi ni chanzo kikuu cha mapato ya nchi kwa ajili ya maendeleo, na Serikali inao wajibu mkubwa wa kuhakikisha kwamba Wafanyabiashara, Wakulima na Wafanyakazi wanalipa kodi kwa mujibu washeria ili Serikali iweze kukusanya kodi kwa ufanisi mkubwa ni lazima kuwe na ofisi za TRA katika maeneo mbalimbali nchini:-

(a) Je, Serikali haoni umuhimu wa kuwa na Ofisi ya TRA katika Wilaya ya Kilindi;

(b) Kwa kutokuwa na Ofisi za TRA Serikali haioni kama inadhoofisha maendeleo ya Wilaya hususani katika suala la mapato;

(c) Kwa kuweka Ofisi ya TRA Wilaya ya Handeni na kuacha Wilaya ya Kilindi Serikali haoni kama inawajengea wananchi tabia ya kukwepa kulipa kodi kutokana na umbali uliopo kati ya Wilaya hizo mbili.

**WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

**126. MHESHIMIWA DAIMU IDDI MPAKATE (TUNDURU KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Katika wilaya ya Tunduru kuna miradi mingi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia ambayo imesimama kwa muda mrefu bila kukamilishwa na wakandarasi kwa sababu ya ukosefu wa fedha:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha za kumaliza miradi hiyo ambayo Wananchi wanajua kuwa fedha zilizotolewa na benki ya dunia lakini haijulikani zilienda wapi.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**127. MHESHIMIWA WILLY QULWI QAMBALO (KARATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Barabara ya Oldeani Junction – Mang'ola - Matala – Manuzi ni kiungo muhimu sana kwa kuunganisha Kanda ya Kaskazini (Mkoa wa Arusha) na Mikoa ya Kanda ya Ziwa (Simiyu):-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami ili iweze kupitika muda wote.

**128. MHESHIMIWA MWANNE ISMAIL MCHEMBA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Hali ya kipande cha barabara kutoka Chaye – Tabora ni sehemu ya barabara ya kutoka Urambo - Kaliua:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara hizo utakamilika.

129. **MHESHIMIWA SHABANI OMARI SHEKILINDI (LUSHOTO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Barabara ya kutoka Mlalo kupitia Ngwelo – Mlola – Makanya – Mlingano – Mashewa ni ya muda mrefu sana na ipo chini ya Halmashauri licha ya kwamba barabara hiyo ni kichocheo cha uchumi kwa majimbo manne:-

Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuipandisha hadhi barabara hiyo na kuwa chini ya TANROADS.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA** **DKT. T. D. KASHILILAH**
**09 MEI, 2016** **KATIBU WA BUNGE**

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA